





KONGAMANO LA FURSA ZA KILIMO BIASHARA




1

Azolla

2

Hydroponic Fodder

3

Hydroponic Vegetable

VIWANJA VYA NYAKABINDI, BARIADI - SIMIYU TAREHE 6/8/2019

Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF)

ikishirikiana na Wakuu wa mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Mara (kanda ya ziwa mashariki), Wizara zenyenye dhamana ya kilimo, uvuvi na ufugaji pamoja na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), wameandaa kongamano la fursa za kilimo biashara litakalofanyika sambamba na maonesho ya Nane Nane katika viwanja vya Nyakabindi, wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu siku ya tarehe 6/8/2019 kuanzia saa tatu asubuhi. Kongamano litafunguliwa na **Waziri Mkuu Mstaifu, Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda**.

Katika kongamano hilo, kutakuwa na mawasilisho ya tafiti zilizofanywa na wadau mbalimbali zinazobainisha fursa nyingi katika sekta ya kilimo cha kisasa (smart farming) ambacho kinajumuisha: Kilimo cha Fodder, Azolla, Kilimo cha Mboga Mboga katika Shamba Kitalu, Ufugaji wa Kisasa wa Samaki Katika Mabwawa, Vizimba, Matanki na Ufugaji wa Nyuki.

Mada zitakazotolewa ni pamoja na:-

- Mafunzo ya kilimo katika eneo dogo kwa kutumia shamba kitalu (**Greenhouse**)
- Mafunzo ya kilimo cha malisho ya wanyama bila udongo (**Hydroponic Fodder**)
- Mafunzo ya kilimo cha mboga mboga bila udongo (**Hydroponic Vegetable**)
- Kilimo cha Azolla kwa ajili ya malisho ya mifugo na mbolea
- Ufugaji wa kisasa wa samaki kwa kutumia vizimba, matanki na mabwawa
- Ufugaji wa kisasa wa nyuki
- Ufugaji wa kisasa wa kuku
- Usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi.
- Mafunzo ya ujasiliamali kwenye mnyororo wa thamani wa kilimo, ufugaji na uvuvi.
- Mikopo na mitaji katika sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi

USHIRIKI NI BURE, KARIBU UELIMIKE

Kutakuwa na wasilisho la fursa za uwekezaji zilizoainishwa katika miongozo ya uwekezaji katika mikoa ya kanda ya ziwa.

Kutakuwa pia na mafunzo ya nadharia na vitendo kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi yatakayofanyika tarehe 2, 4 na 5/08/2019 sambamba na maonesho ya Nane Nane.